**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dodoma*
*12 Machi, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS SAMIA APOKEA TAARIFA ZA TUME ZA KUTATHMINI MIGOGORO YA ARDHI NA ZOEZI LA UHAMAJI WA HIARI KATIKA ENEO LA HIFADHI YA NGORONGORO

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amepokea rasmi taarifa za Tume ya Kutathmini Mgogoro wa Ardhi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, pamoja na Tume ya Kutathmini utekelezaji wa zoezi la Uhamaji wa Hiari kwa wakazi wa eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Rais Dkt. Samia amesema Ngorongoro ni maliasili adhimu inayopaswa kulindwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho, kwa umuhimu wake wa kipekee katika uhifadhi wa bioanuai, utalii, historia ya mwanzo ya mwanadamu na utamaduni wa jamii za wakaazi wa asili wa eneo hilo.

Ameongeza kuwa, Serikali ina wajibu wa kulinda mfumo wa ikolojia unaounganisha Hifadhi ya Ngorongoro, maeneo ya Loliondo na Ziwa Natron, na kufafanua kuwa zoezi la uhamaji wa hiari lilianzishwa kwa nia ya kulinda mfumo huo wa ndani ya eneo la hifadhi, wenye manufaa makubwa kwa utalii wa nchi na urithi wa dunia.

Aidha, amebainisha kuwa Serikali itaendelea na utekelezaji wa zoezi la uhamaji wa hiari kwa kurekebisha kasoro zilizobainika katika awamu ya kwanza na kuboresha mfumo wa uratibu na utekelezaji wake, kama sehemu ya kulinda uhifadhi wa mazingira ya asili ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, sambamba na kuimarisha ustawi wa wananchi wakaazi wa asili wa eneo hilo.

Akiwasilisha ripoti ya Tume ya Kutathmini Mgogoro wa Ardhi katika eneo la Ngorongoro, Mwenyekiti wa Tume hiyo amebainisha kuwa ongezeko la watu, mifugo na makazi ndani ya eneo la Ngorongoro limeongeza shinikizo la matumizi ya ardhi na kusababisha changamoto za kimazingira, migongano kati ya binadamu na wanyamapori pamoja na kupungua kwa baadhi ya rasilimali za asili.



Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano / ikulu_Tanzania / ikulu Tanzania / ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania

Tume imependekeza hatua mbalimbali za utatuzi ikiwemo mapitio ya baadhi ya sheria, kuimarisha usimamizi wa maeneo ya hifadhi na kuweka mikakati ya maendeleo ya jamii nje ya eneo la hifadhi.

Halikadhalika, sehemu ya ripoti ya Tume ya Kutathmini Uhamaji wa Hiari imeeleza kuwa utekelezaji wa zoezi hilo haukufikia matarajio kutokana na changamoto za uratibu, ushirikishwaji wa wananchi, pamoja na mabadiliko ya baadhi ya miongozo ya utekelezaji, na kushauri kuwa zoezi hilo ni la msingi na linaweza kufanikiwa kwa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa.

Rais Dkt. Samia amesema Serikali imepokea mapendekezo ya tume zote mbili na itayafanyia kazi kwa lengo la kupata suluhu ya kudumu kwa lengo la kulinda maslahi ya wananchi, uhifadhi wa mazingira na ustawi wa taifa. Aidha, ameielekeza Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) kusimamia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na tume zote mbili, pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi kuratibu utekelezaji huo.



Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu